



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

TAARIFA KWA UMMA  
KUHUSU RATIBA YA UCHAGUZI MDOGO WA  
UDIWANI KATIKA KATA SITA (6) ZA TANZANIA BARA

Tume ya Taifa ya Uchaguzi imepokea taarifa kutoka kwa Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa ambaye kwa kutumia mamlaka aliyopewa chini ya Kifungu cha 13(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 ameitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata sita (6) zilizopo katika Halmashauri sita(6) za mikoa sita ya Tanzania Bara. Nafasi hizo wazi zimetokana na vifo vya Madiwani watano (5) na mmoja (1) kujiuzulu.

Kwa kuzingatia matakwa ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292 Tume ya Taifa ya Uchaguzi inatoa taarifa kwa Umma kuhusu uwepo wa Uchaguzi Mdogo wa Madiwani katika Kata hizo.

Tume imepanga kuendesha Uchaguzi huo Mdogo wa Madiwani kwa kuzingatia ratiba ifuatayo:

1. Fomu za Uteuzi wa Wagombea zitatolewa kati ya tarehe 15 hadi tarehe 19, Aprili mwaka huu.
2. Uteuzi wa Wagombea utafanyika tarehe 19, Aprili mwaka huu.

3. Kampeni za Uchaguzi zitafanyika kuanzia tarehe 20, Aprili hadi tarehe 18 Mei mwaka huu.

4. Siku ya Uchaguzi itakuwa ni tarehe 19 Mei mwaka huu.

Uchaguzi katika Kata hizo, utafanyika sambamba na Uchaguzi Mdogo wa Ubunge katika Jimbo la Arumeru Mashariki.

Tume inapenda kuvikumbusha Vyama vya Siasa na wadau wote wa Uchaguzi kuzingatia Sheria, Kanuni, Maadili ya Uchaguzi, Taratibu, Miongozo na Maelekezo yanayotolewa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi wakati wa kipindi chote cha Uchaguzi huu mdogo.

Kata zilizowazi na Halmashauri zake ni kama ifuatavyo:-

N°	Mkoa	Halmashauri	Kata
1.	Katavi	Mpanda	Uwanja waNdege
2.	Kagera	Missenyi	Kitobo
3.	Mbeya	Kyela	Kyela
4.	Dar es Salaam	Kinondoni	Mikocheni
5.	Lindi	Lindi	Mvuleni
6.	Dodoma	Chamwino	Manda

Imetolewa leo tarehe 8 Aprili, 2019.

Jaji (R) Semistocles S. Kaijage

**MWENYEKITI**

**TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI**